**MADA NA. 6 – Kilimo Kwanza. Tutarajie Nini?**

***6.1 Wasilisho la Mada kutoka Baraza la Taifa la Biashara, Tanzania* – Bw. Felix Mosha**

*"Kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya Tanzania, kilimo ni kila kitu"* Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati akizundua **KILIMO KWANZA, tarehe 3 Agosti, 2009 mjini Dodoma - Tanzania**

Unapomuuliza wananchi "Kilimo Kwanza" unapata majibu tofauti. Kilimo ni azma iliyoamuliwa kitaifa ili itupeleke katika mapinduzi ya kijani. Kilimo kwanza kinajumuisha uzalishaji wa kawaida katika ***kilimo, mifugo, misitu na uvuvi***.

***Kwa nini Kilimo Kwanza ni muhimu:***

- kwa siku zote na vitu vyote tulivyofanya, taifa hili haliwezi kujilisha lenyewe. Kitu cha kwanza ni lazima tujitosheleze kwa chakula chetu wenyewe. Sasa hivi tunazalisha asilimia 90 tu ya mahitaji yetu, wakati tunatakiwa tufikie asilimia 120, kwa maana ya ziada.
- ndio nguzo kuu ya kufikia Dira 2025 na msukumo wa kufikia malengo ya taifa ya maendeleo, kijamii na kiuchumi .
- hakuna taifa lililoweza kuendelea kiuchumi bila kilimo cha kisasa
- hakuna taifa lililopunguza umasikini bila tija katika kilimo
- asilimia 95 ya watu wetu wanategemea kilimo kama njia ya maisha. Lazima uanze na kilimo ili uwanasue.
- bei za chakula zinachangia asilimia 55.9 katika mfumuko wa bei.

Palikuwepo na juhudi nyingi huko nyuma za kuinua kilimo, ikiwemo Kilimo cha Kufa na Kupona, Siasa ni Kilimo, n.k. lakini hazikuweza kubadilisha mfumo mzima wa kilimo. Juhudi za nyuma zilikuwa na msukumo zaidi wa serikali kuu, safari hii sekta binafsi ndio kichocheo kikuu. Mataifa yaliyoendelea yanazalisha kile ambacho wanakitumia, tofauti na nchi za kusini. Taifa linatakiwa lianze kuzalisha mazao yanayoyatumia na yenye soko. Ili tuweze kuleta ***mapinduzi ya kijani***, tunahitaji mambo yafuatayo:

- mbegu bora – tunahitaji wastani wa tani 120,000
- mbolea bora – mbolea tunayotumia ni kidogo sana. Mataifa yaliyoendelea yanatumia kilo 120 kwa hecta; Afrika Kusini tani 50/hecta, Malawi kilo 127/hecta, wakati Tanzania ni kilo 9 tu kwa hecta!
- vifaa vya kisasa pamoja na madawa – tulikuwa na trekta 17,000 kitaifa na sasa hivi zipo 8,000. Kuna mikoa ina trekta 5 tu! Tunahitaji trekta angalau 20,000. Jembe la mkono no asilimia 70 ya kilimo chetu, maksai asilimia 20 na trekta asilimia 10.

***Changamoto:***

- Usindikaji wa mazao – nchini Malaysia wanasindika asilimia 83 ya mazao yao, Thailand asilimnia 78, na Tanzania asilimia 1 tu.
- Fedha – kilimo kipate uwekezaji wa muda mrefu (long-term financing) ambao wakulima wataumudu. Serikali iharakishe kuanzisha Benki ya Wakulima ambayo itatoa mikopo ya muda mrefu kwa wakulima katika riba ndogo.

- Sera za serikali zimvutie mkulima – kodi nafuu!
- Kilimo cha umwagiliaji – Tanzania inamwagilia asilimia 1 tu ya ardhi ya kilimo wakati hecta milioni 29 zinaweza kumwagiliwa. Tanzania ni taifa lenye maji zaidi Afrika ukiacha DRC.
- Mifugo, Uvuvi, Misitu na Nyuki – zaidi ya ng'ombe milioni 19, ambazo tungeweza kuziongeza thamani. Tanzania ina asilimia 50 ya Ziwa Victoria na Kenya asilimia 6, lakini Kenya wanasafirisha minofu mingi zaidi kuliko sisi. Tunahitaji mikakati wa kurekebisha haya.

Kwa kumalizia naweza kusema kwamba kilimo cha Tanzania, cha mkulima mkubwa na mdogo, kiwe kilimo cha biashara. Hiki ni kilimo cha kila mtu. La muhimu ni tija. Bila ya mapinduzi ya kijani taifa hili halitaendelea.

***6.2 Mchango kutoka Action Aid* – Elias Utinda**

Tanzania ina mikakati mizuri lakini tatizo ni utekelezaji. Bajeti za Kilimo/Mifugo/Uvuvi – je bajeti hizi zinalenga kumuondolea adha mkulima? Azimio la Maputo lililenga kwamba bajeti za nchi za Afrika ziweke kiwango cha chini cha asilimia 10 kwa ajili ya kilimo, Tanzania ni asilimia 7 tu. Serikali ipange vizuri bajeti hii ili imfikie mkulima. Nchini Malawi ambako kuna mapinduzi ya kijani, bajeti ya kilimo imeongezwa na hivyo kuongeza matumizi ya mbolea.

Katika uwekezaji, nchi lazima ijipange kukabiliana na changamoto ya kuzalisha nishati-mimea (bio-fuel) ambayo hutumia ardhi kubwa ambayo ingeweza kutumika kwa kilimo cha chakula. Masoko ya mazao yetu yako vipi?

***6.3 Maoni kutoka PELUM* – Bw. Simon Mwang'onda**

Tanzania inafuata siasa gani kwa sasa, ujamaa au ubepari? Vivyo hivyo, Kilimo Kwanza kinafuata siasa zipi? Mlengwa katika kilimo kwanza ni nani, ni huyu Mtanzania masikini, anayeishi chini ya dola mbili kwa siku au ni mwekezaji kutoka nje?

Iwapo tunamlenga mkulima masikini, tuna mikakati gani ili kumsaidia kuzalisha na kilimo chake kiwe na tija?

Soko huria – unakuta serikali inamzuia mkulima asiuze mahindi yake eti kwa sababu ya tishio la njaa, je imefikiria kuhusu gharama zake za uzalishaji?

Elimu ya Mtanzania imeshuka sana, Je, mkulima ataweza kupiga hesabu ya biashara yake ya kilimo ili asipate hasara?

Mwisho, bila kushughulikia matatizo ya ufisadi na rushwa hatutafanikiwa.

***6.5 Uzoefu kutoka The Eastern and Southern Africa Small Scale Farmers Forum* – Joe Mzinga**

- Kilimo kipo nyuma sana
- Kilimo Kwanza hakitekelezwi, wadau wanatakiwa waipokee hoja na kuifanyia kazi
- Tufuate nguzo kumi za kilimo bora
- Pawepo pia utashi wa kisiasa
- Fikra na mtazamo kuhusu kilimo unapaswa kubadilika.

*6.6 Mchango kutoka Chuo Kikuu, Mzumbe* **– Dk. Prosper Ngowi**

Changamoto za Kilimo Kwanza:

- Changamoto kubwa ni upatikanaji wa fedha. Benki za kilimo zianzishwe ambako wakulima wanaweza kuweka fedha na pia kupewa mikopo. Benki za biashara zizikopeshe benki za kilimo.
- Sekta binafsi iwekeze katika kilimo.
- Kuwepo kwa utashi wa kisiasa na kiuchumi kutasaidia kupunguza au kumaliza kabisa changamoto katika kilimo

***6.7 Mjadala wa Pamoja, Maoni na Mapendekezo***

- Kilimo kwanza bado kina changamoto nyingi ambazo kutokana na mdororo wa uchumi duniani baadhi ya malengo yaliyokusudiwa yameshindwa kutekelezwa
- Kilimo Kwanza kingekuwa sera ya kufufua kilimo cha umwagiliaji basi kingefanikiwa kwa kiasi kikubwa badala ya kutegemea mvua ambazo mara nyingi hazinyeshi.
- Je, serikali itatumia mbinu gani kuwezesha kilimo kiwe imara?
- Mbona kuna asasi chache zinazohusika katika kilimo?
- Watu wengi wangependa kushiriki katika Kilimo Kwanza, lakini ardhi kubwa zinapokonywa na serikali, je sera za kilimo kwanza zinazungumziaje suala hili?
- Ufafanuzi unahitajika kati ya wakulima na wafugaji
- Wakulima wamekuwa watu wa kupangiwa bei
- Mkulima aliye kijijini hana uwezo, je, kuna mikakati gani ya kumwezesha kununua '*power tiller*' la milioni tisa?
- Sera hii ikitekelezwa vizuri itawakomboa wananchi wengi ambapo zaidi a Watanzania asilimia 80 wanategemea kilimo.
- Wananchi wapatiwe mashamba makubwa ili wazalishe
- Wakulima wapatiwe pembejeo na madawa ya kilimo ili wazalishe – trekta, mbolea.
- Usindikaji wa mazao utiliwe mkazo ili kuinua thamani ya mazao yetu ambayo mengi husafirishwa ghafi na kuzinufaisha nchi za nje.
- Serikali imejiandaa vipi na wanasiasa wanaoharibu miradi ya kilimo?

Mtoa mada alikuwa na haya ya kuchangia:

- Ili Kilimo Kwanza kifanyike, kila kiongozi lazima alime. Pia Kilimo Kwanza sio siasa bali ni utaratibu wa kitaalamu ulioletetwa na sekta binafsi
- Maeneo ya ufugaji na kilimo yatatengwa rasmi kutokana na mpango mzima wa Kilimo Kwanza hivyo kupunguza migogoro
- Mkopo wa mkulima mmoja mmoja ni mgumu, ila itakuwa rahisi kwa kupitia SACCOS ambazo zitapewa mikopo moja kwa moja kutoka benki

- Wanafunzi wanaosomea kilimo wapewe ‘full sponsorship’ katika masomo yao. Pia elimu itolewe kwa wakulima nwetu katika matumizi ya mbolea, madawa, mbegu bora, n.k.
- Kupitia kilimo, nchi yetu inaweza kuendelea na kukua kiuchumi haraka, kama ilivyo nchi ya Malawi.